

JINA.....

SHULE.....

NAMBARI.....SAHIHI.....

TAREHE.....

**KISWAHILI**

102/3

**MUHULA WA TATU**

Muda : Saa 2 ½

MEI/JUNI 2021

**MTIHANI WA DIRA 39**

**KIDATO CHA TATU**

**MTIHANI WA KWANZA, MUHULA WA TATU**

**Maagizo:**

1. Jibu maswali yote. Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.

**Kwa matumizi ya mtihani pekee.**

Swali	Upeo	Alama
1	20	
3	20	
4	20	
<b>Jumla</b>	<b>60</b>	

## **SEHEMU YA KWANZA: USHAIRI-ALAMA 20**

### **1. Soma shairi hili kwa umakini kisha ujibu maswali.**

U wapi ujana wangu, na madhubutu ya nia?

Niko hapa peke yangu, ujana umepotea

Umeanacha na machungu, mambo niliyozoea

Kuwa na uwezo wangu, leo hayawezi kuwa

Afya ya ujana wangu, nayo imeshika njia,

Siku za ujana wangu, nazo sizioni pia,

Nadhari sasa si yangu, tazama hii dunia!

U wapi ujana wangu, ubingwa na mazoea

Ndugu za jamaa zangu, na waty waliojua

Wamehama ulimwengu, ni pweke nimebakia

Nguvu wanazo wenzangu, sasa wanazitumia

Ni kishikacho si changu, ajabu hii dunia

Hutia kizunguzungu, wakati wa kuchungua

Kama hukumbuki Mungu, kufuruni utakuwa.

U wapi ujana wangu, na maringo ya tabia?

Hamna kinywani mwangu, jino lililobakia,

Na laini gumu kwangu, sina cha kutafunia

Kitamu sasa kichungu, hata kama ni halua

Kama ningefungwa pingu, sina la kufurahia

Katika maisha yangu, nimebaki na fadhaa

Kama fumbo ulimwengu, na watu wazuzuliwa.

(S. Robert)

## **Maswali**

- a. Bainisha kwa hoja tano kinyume kinavyojitokeza katika shairi hili. alama 5
- b. Eleza muundo wa shairi hili. alama 4
- c. Eleza aina nne za taswira katika shairi hili. alama 4
- d. Onyesha mifano ya binu zifuatazo katika shairi hili. alama 4
  - (i) Kweli kinzani
  - (ii) Tashihisi
  - (iii) Tafida
  - (iv) Usambamba
- e. Bainisha nafsini katika shairi hili. alama 1
- f. Eleza toni ya shairi hili. alama 1

## **SEHEMU YA B: TAMTHILIA-ALAMA 20**

### **KIGOGO-P.KEA**

2. Eleza umuhimu wa mazungumzo baina ya Majoka na Ashua ofisini. Alama 10
3. Fafanua umuhimu wa madhari ya ofisini mwa Majoka. Alama 10.

## **SEHEMU YA C: FASIHI SIMULIZI-ALAMA 20**

4. Jadili namna wanafunzi wanavyoweza kuendeleza fasihi simulizi katika maeneo ya shuleni. Alama 20